KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 20, Issue 5

7th Jumaadal Awwal 1433

30th Mar, 2012

MIUJIZA YA MTUMЄ MUHAMMAD (صلى الله عليه وسلم)

Al-hidaaya.com

"Ametakasika, Aliyemchukua mja Wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao Tumevibariki vilivyouzunguka, ili Tumwonyeshe baadhi ya Ishara Zetu. Hakika ni Mwenye Kusikia na Mwenye Kuona." (Al-Israa 17: 1)

UTANGULIZI:

Allaah (سبحانه وتعالى) Anaelezea Utukufu Wake, Ukubwa Wake na Uwezo Wake, kuwa Yeye ni Mweza wa kila kitu na Anafanya kila kitu Anachotaka kukifanya. Yeye pekee Ndiye Mungu wa kweli na Yeye pekee Yake Ndiye Mlezi (Muumba, Mtoaji wa Riziki na Mwenye kutoa ukimu wa kila kiumbe). Alimchukua mja Wake Muhammad (صلى الله عليه وسلم) kutoka Makkah na kumpeleka katika msikiti wa mbali huko Jerusalem katika usiku mmoja. (Kutoka Tafsiyr ya Ibn Kathiyr)

MIUJIZA YA MTUME WA ALLAAH (صلى الله عليه وسلم)

QUR-AAN

Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipewa miujiza mingi na Mola wake. Muujiza wake mkubwa ni Kitabu cha Qur-aan, kitabu ambacho kiliteremshwa miaka 1400 iliyopita na hakuna hata mtu mmoja ambaye ameweza kubadilisha hata herufi moja au kuleta kitabu cha mfano wake. Allaah Amesema: "Hakika Sisi ndio Tulioteremsha Ukumbusho na hakika Sisi ndio Tutaoulinda" (Al-Hijr 15: 9).

Aayah hii ni changamoto dhidi kwa makafiri kuwaambia kitu kinachofanana na Qur-aan ambao walijaribu kufanya mifano ya Qur-aan wakawa wameshindwa vibaya sana. Vitabu vingine vya kutoka Kwa Allaah (سبحانه وتعالى) Taurati na Injili ambavyo viliharibiwa na kubadilishwa na ujumbe kubadilika ama kwa kuongeza maneno au kupunguza maneno na maana vile vile. Allaah Amesema juu ya Qur-aan kuwa "Atailinda" na kweli Ameilinda na Ataendelea Kuilinda.

Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema, "Kila mtume aliyekuja kabla yangu alipewa muujiza na miujiza hiyo ilibakia kuwa miujiza wakati wa uhai wao hao mitume.: Mfano 'Iysa (عليه السلام) alikuwa na muujiza wa kutibu watu wagonjwa na kufufua wafu Musa (عليه السلام) alipewa fimbo ya miujiza na mambo mengine, nami nimepewa muujiza wa milele, Qur-aan itabakia kuwa muujiza hadi kusimama Qiyaamah. Hivyo natarajia kuwa wafuasi wangu watakuwa ni wengi katika idadi zaidi ya wafuasi wa Mitume wengine kwa kuwa muujiza wangu utabakia na utakuwepo hadi Siku ya Qiyaamah ambao ni Qur-aan. Kila anayekisoma Kitabu hiki hata kama ni mpagani basi yeye huvutika na kuona ukweli uliomo ndani yake na kuona hakuna aliyekiandika isipokuwa Bwana wa Mbingu na Ardhi." (Swahiyh Al-Bukhaariy na Swahiyh Muslim)

KUPASUKA KWA MWEZI

Muujiza mwingine wa Mtume wa Allaah ilikuwa ni kupasuka kwa mwezi. Anas anasema katika riwaya yake, kuwa watu wa Makkah walimtaka Mtume (صلى الله عليه وسلم) awaonyeshe muujiza na akawaonesha kupasuka kwa mwezi. (Swahiyh Al-Bukhaariy, Juzuu ya 4 Namba 831)

KUTOKA MAJI KUTOKA VIDOLE VYA MTUME (صلى الله عليه وسلم)

Imepokewa kutoka kwa Jaabir ibn Abdullah akisema: "Nilikuwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) na muda wa kuswali Swalah ya Al-'Aswr ukafika. Tulikuwa hatuna maji isipokuwa maji kidogo tu ambayo yalikuwa ndani ya chombo ambayo yaliletwa kwa Mtume. Basi aliweka mkono wake ndani ya maji hayo na kutandaza vidole vyake na huku akisema, "Njooni Haraka watu wote ambao wanataka kutawadha Hii ni baraka kutoka kwa Allaah" Nikaona maji yakibubujika kutoka katika vidole vyake. Hivyo watu walitawadha na wengine wakawa wanakunywa maji hayo na mie nilitaka kunywa maji mengi kupita kiasi (kwa sababu nilijua kuwa ilikuwa ni baraka). Mpokeaji wa hadiyth hii kutoka kwa Jaabiri alisema kuwa nilimwuliza Jaabir Je, mlikuwa watu wangapi wakati huo? Akajibu, "Tulikuwa watu elfu moja na mia nne." (Swahiyh Al-Bukhaariy Juzuu 7 namba 543 na Swahiyh Muslim Juzuu 4 namba 779). Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa amepewa miujiza mingine mingi. Muujiza mwingine mkuu ni ule wa Israa na Mi'iraaj au "Safari ya Usiku" Makala hii ni kujaribu kuonesha faida zinazopatikana katika safari hii na mafunzo yanayopatikana katika muujiza huu mkubwa. Tukio la Israa na Mi'iraaj lina hekima kubwa sana na mafunzo makubwa. Funzo lake kubwa ni kuwa mja hapaswi kukata tamaa, lazima awe daima anamtegemea Mola wale na atamletea faraja hata kama kutakuwa na mambo mazito yanamkabili. Zaidi ya hapo mwanadamu anapaswa kuwa daima karibu na Mola wake hasa wakati anapokuwa anakabiliwa na mambo mazito na vitendo vya kuhuzunisha au mikasa mizito, kwani matatizo hayo hupotea kama vile yalikuwa hayajatokea.

MWAKA WA HUZUNI

Tukio la Israa na Mi'iraaj lilikuwa katika kipindi cha mwaka wa huzuni. Mwaka huu ulipewa jina hilo kutokana na sababu zifuatazo:

1- Kifo cha 'Ami ya Mtume, Abu Twaalib. Abu Twaalib alikuwa ni mlinzi na mlezi wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakati Waislamu wakiwa Makkah na yeye alimkinga dhidi ya mashambulizi ya makafiri wa Makkah. Watu wa Makkah walipopinga ujumbe wa Muhammad kwa nguvu na kuanza

YALIYOMO

MIUJIZA YA MTUMЄ 1 - 4

kumshambulia Mtume na Waislamu, Abu Twaalib alikinga kifua chake na kumhami mtoto wa nduguye. Alisema, "Tunapenda kusaidia tunakubali ushauri wako na tunayakubali maneno yako. Hawa ni watu wa jamii yako ambao umewakusanya na mimi ni miongoni mwao, lakini mimi ni mwepesi kuliko wote kufanya kile ukitakacho. Fanya kila lile uliloamriwa kufanya. Nitakulinda na kukuhami, lakini siwezi kuiacha dini yangu" Abu Lahab akapayuka: "Wallaahi jambo hili ni jambo ovu Wewe lazima umkataze hayo ayafanyayo kabla ya watu wengine hawajamkanya". Abu Twaalib akasema, Naapa nitaendelea kumlinda na kumhami katika maisha yangu yote". (Ar-Rahiyqul -Makhtuum).

Ameeleza Al-'Abbaas bin Abdul-Mutwalib (رضي الله عنه) kuwa alimwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم), "Hukuwa mwenye kumsaidia 'Ami yako, Abu Twaalib, japo kuwa yeye alikuwa ni mtu mwenye kukuhami sana na alikuwa anachukizwa sana kwa mambo uliyokuwa unatendewa na Makureshi." Mtume akasema, "Yuko katika moto mwepesi, kama si mimi angelikuwa kwenye moto wa tabaka la chini kabisa huko Jahanam." (Swahiyh Al-Bukhaariy Juzuu 5 Namba 222); Hivyo Abu Twaalib licha ya kuwa kafiri alimuunga mkono Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa nguvu zake na mali zake dhidi ya makafiri. Wakati Abu Twaalib alipokuwa hai makafiri walikuwa hawawezi kumdhuru Mtume (صلى الله عليه وسلم) . Hata hivyo, kifo cha Abu Twaalib kilikuwa ni mwanya mwa makafiri wa kuendeleza vitimbi vyao dhidi ya Mtume pamoja na Waislamu kwa ujumla. Tabia yao ya ukatili ilimfanya Mtume aone maisha mjini Makkah ni magumu. Kutoa shahada kwa Maswahaba wa Mtume mjini Makkah ilikuwa ni njia ya kujitangazia uadui wa wazi wazi na wakawa wanapata madhila na kuadhibiwa vibaya. Kila aliyesilimu aliambiwa afanye moja kati ya mambo mawili: aritadi au aondoke hapo nchini au sivyo basi roho yake itafariki dunia; makafiri hawakutaka njia nyingine zaidi ya hiyo. Lakini Maswahaba licha ya kuwa hiki kilikuwa ni kipindi kigumu sana na chenye taabu kubwa sana katika maisha yao kutokana na adhabu na madhila waliyoyapata, waliendelea kusimama imara juu ya imani ya Uislamu na walisonga mbele na Mtume wao katika msimamo huo. Kupanuka kwa Uislamu kuliwaudhi sana makafiri na wakajaribu kila njia ili kuzuia na kukinga Uislamu usiwepo katika nchi yao. Ulinganiaji wa dini hii ukawa mzito kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na hata kuishi mjini Makkah ikawa ni hali ngumu sana kwake na kwa Waislamu.

2- Kifo cha mama wa Waumini Khadiyjah (رضي الله عنها) Ni miezi miwili tu baada ya kifo cha Abu Talib, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipata tatizo lingine zito lililomhusu yeye binafsi. Mke wake na Mama ya waumini, Bi Khadiyjah (رضي الله عنها) alifariki. Mama huyu, mama wa Waumini Khadiyjah, alikuwa ni rehma kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى). Daima alikuwa na Mtume wakati akipata madhila na maudhi ya makureshi na alikuwa naye siku zote wakati wa mitihani mizito ilipokuwa inamwendea Mtume kutoka kwa mahasimu wake wa Kikureshi na walikuwa pamoja katika hali hiyo kwa muda wa miaka 25. Na kwa yote hayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa ukaribu huo aliokuwa nao mama wa Waumini Khadiyjah alisikitika sana kwa kifo cha mkewe mpenzi na kuna wakati alisikika akisema juu ya bibi huyu, "Aliniamini wakati wengine hawakufanya hivyo, Alijiunga na Uislamu wakati watu walikuwa hawataki kufanya hivyo. Pia alinisaida na kuniliwaza mwenyewe na na kwa mali zake wakati kulikuwa hakuna hata mtu wa kuniunga mkono. Pia nilipata watoto kutoka kwake.'' (Musnad Ahmad 6/118).

Matukio haya mawili yalitokea mfululizo. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa amefikia hali ya kubabaika namna gani awaongoze Waarabu wa Makkah, basi aliangalia upande wa Twaaif mji ambao kwa wakati huo ulikuwa unahitajia msaada na uongozi. Lakini hata huko pia hakupokelewa na hali hiyo kuongeza machungu moyoni mwake (صلى الله عليه وسلم) hata akaona kipindi hicho kuwa ni "Mwaka wa Huzuni".

Katikati ya huzuni zote hizo Allaah Alimchukua mja Wake katika muujiza mkubwa wa Israa na Mi'iraaj ili amwoneshe Aayah Zake na kumpatia msaada na himaya. Allaah Anasema, "Ili Tumwoneshe baadhi ya Ishara Zetu…"

Kwa muujiza wa Israa na Mi'iraaj , Allaah Aliweka msingi kwa waja Wake kuwa hata kama makafiri wangelifunga mlango wa Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم), Allaah Ndiye Mwenye Kumhami na ndio Mlezi Wake na milango ya Peponi iko wazi kwa ajili ya Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Hakuna nguvu ambayo inaweza kumteza au kumdhuru yule ambaye yuko chini ya ulinzi wa Allaah. Israa na Mi'iraaj ilikuwa ni dalili ya kuonesha kufanikiwa kwa Da'wah ya Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) na ushindi wake juu ya maadui zake pamoja na kuwepo kwa matatizo na huzuni zote hizo.

SAFARI YA ISRAA

Lini kilikuwa Kipindi cha Israa na Mi'iraaj? Tarehe hasa ya tukio la Israa na Mi'iraaj haifahamiki kwa uhakika. Ibn Kathiyr amenukuu kutoka kwa wanachuoni mbali mbali katika kitabu chake Al-Bidaayatu wan-Nihaayah (3/108) juu ya terehe ya tukio hilo. Wanachuoni wengi wanaona kuwa tarehe hiyo ilikuwa kati ya miezi 12 na 16 kabla ya Hijra yake kwenda Madiynah. Na wa zaidi ya hapo wamekhitilafiana juu ya siku na hata huo mwezi.

KABLA YA SAFARI

Malaika Jibril (عليه السلام) alifungua kifua cha Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم), akatoa moyo wake na kuuosha kwa maji ya Zam Zam. Anasema Anas Bin Maalik ((رضي الله عنه: "RasuluLlaah (صلى الله عليه وسلم) alichukuliwa katika Israa na Mi'iraaj kutoka Msikiti Mtukufu wa (Makkah) Ka'abah. Watu watatu walimjia (ndotoni) akiwa amelala ndani ya Msikiti wa Makkah kabla Wahyi haujaletwa kwake. Mmoja wao akasema: "Ni yupi kati ya hawa watu?" Malaika wa kati akasema "Yule ambaye ni mbora kuliko wote" na Malaika wa Mwisho akasema, "Chukueni aliye mbora wao". Mambo haya yalitokea katika usiku huo huo. Usiku huo hakuwaona, lakini aliwaona usiku mwingine ambapo tayari wahyi ulikuwa umeletwa kwake na alikuwa macho amelala lakini alikuwa hadhiri (Ni kawaida ya Mitume wote kulala macho wakati wako hadhiri). Wale Malaika hawakumsemesha bali walimbeba hadi wakamfikisha katika kisima cha Zam Zam. Miongoni mwao Jibril (عليه السلام) alikuwa akiongoza na kuelekeza kifanyike nini.

Alipasua sehemu kati ya koo na kati ya kifua na akatoa vyote vilivyokuwemo kifuani na kuviosha kwa maji ya Zam Zam kwa mikono yake mwenyewe na pia kusuuza sehemu za ndani za mwili na kisha kikaletwa chano cha dhahabu kikiwa na bakuli la dhahabu kililetwa ndani ya bakuli mkiwa mkajazwa imani na busara. Jibril (عليه السلام) akachukua vitu hivyo kutoka ndani ya bakuli na kuvijaza kifuani mwa Mtume kisha akachukua viungo vya Mtume pamoja na mishipa ya damu akavijaza kifuani kwa Mtume na kukifunga kifua" Swahiyh Al-Bukhaariy Juzuu 9 Namba 608, na Juzuu 5 Namba 227).

Israa maana yake ni safari ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) yeye akiwa ni mwili

wake na akili zake na roho yake kutoka Ka'abah huko Makkah mpaka Msikiti wa Al-Aqswaa huko Quds (Jerusalem) akiwa amebebwa na mnyama wa ajabu mwenye kuvutia umbo lake anayeitwa Buraaq na kisha safari ya kurejea kwake Makkah.

AL-BURAAQ

Mtume (صلى الله عليه وسلم) alichukuliwa kutoka Msikiti wa Haram, Makkah mpaka Msikiti wa Al-Aqswaa mjini Quds juu ya mnyama aitwaye Al-Buraaq akiwa ameambatana na Malaika Jibril ('Alayhis-Salaam) Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwelezea Al-Buraaq kuwa, "Nililetewa Al-Buraaq, mnyama mrefu wa umbo na mweupe, ni mkubwa kiasi zaidi ya punda lakini ni mdogo kuliko nyumba, ambaye anapokwenda mbio hatua yake ni upeo wa macho yake. Nilimpanda mnyama huyo mpaka nikafika Msikiti wa Al-Aqswaa huko Al-Quds (Jerusalem). Hapo nilimfunga pale mahali ambapo Mitume wengine walikuwa wakifunga wanyama wao." (Swahiyh Al-Bukhaariy na Swahiyh Muslim)

Anas Bin Maalik alisema, "Katika usiku ambao Mtume alipelekwa mbinguni, Al-Buraaq aliletwa kwake akiwa amefungwa vikuku na ana matandiko, lakini alileta ujeuri kidogo, na ndipo Jibril alipomwambia Al-Buraaq "Je unafanya haya kwa Muhammad? Hakuna mtu mtukufu aliyewahi kukupanda ambaye ni mtukufu zaidi ya huyu mbele ya Macho ya Allaah." Kisha akatoa jasho." (At- Tirmidhiy na Musnad Ahmad).

MAANA YA AL-BURAAQ KWA KIARABU NI MWALE UNAOTOKA KATIKA MWANGA

Leo hii, Wanasayansi wanatuambia kuwa mwanga una mwendo kasi zaidi ya vitu vyote duniani. Huenda masafa ya maili 700 milioni kwa saa moja. Miaka 1400 iliyopita wakati ambapo kulikuwa hapajatokea utafiti na uvumbuzi palikuwa hakuna mtu ambaye aliweza hata kukisia mwendo kasi wa mwanga wala ukweli wake ukoje. Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) walimwita mnyama huyo kama Al-Buraaq kwa msingi wa mwendo wake ulivyo na kasi kali.. Huu ni ukweli ambao unthibitisha ukweli wa Uislamu na ukweli wa Utume wa Muhammad (صلى الله عليه وسلم) kama Alivyosema Allaah ndani ya Qur-aan, "Tutawaonyesha ishara Zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli." (Fusswilat 41:53).

Hapo kale watu walipinga na kusema 'mnyama huyo katokea wapi tena ambaye alimchukua Mtume (صلى الله عليه وسلم) kutoka sehemu moja ya dunia mpaka nyingine na kisha kapita naye katika anga za mbingu na tena katika usiku mmoja?" Leo hii tunaona vipando ambavyo vimunda na binadamu, roketi na misali vikita maelfu ya maili kwa muda dakika chache tu. Iwapo mtu ambaye ni kiumbe cha Allaah Muumba wa Ulimwengu, Je, Allaah kwa nini asiumbe mnyama mwenye uwezo wa kukata masafa ya mamilioni ya maili kwa muda mfupi.

Kituo cha kwanza cha Safari - Al-Aqswaa: Mtume alisema: "Kisha niliingia Msikiti wa Al-Aqswaa, nikaswali Raka'ah mbili" (Swahiyh Muslim)

Kuna riwaya nyingine ambazo zinaeleza kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliswali na Mitume wengine hapo msikitini na yeye akiwa Imaam. Msikiti wa Al-Aqswaa umekuwa na sifa ya kuwa ni kituo cha Mitume wote. Toka siku ya Al-Khaliyl Ibrahim(عليه السلام) hivyo Mitume wote walikusanyika hapo na Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) akawa Imaam wao. Hii ni dalili ya nafasi kubwa aliyo nayo Muhammad ambaye ni Mtume wa mwisho miongoni mwa Mitume wengine (عليهم السلام). [Tafsiyr Ibn Kathiyr. Kisa cha Israa na Mi'iraaj kimeelezwa ndani ya Qur-aan (Al-Israa 17:1) Aayah inayofuatia inaeleza matendo ya aibu na makosa ya Mayahudi na kufuatia juu ya hayo makemeo makali ya Qur-aan. Mpangilio huo si kwa bahati tu, Al-Quds (Jerusalem) ilikuwa ni kituo cha kwanza cha safari hii ya Usiku na hapa kuna ujumbe ambao unaelekezwa kwa Mayahudi na kupewa ujumbe kuwa hadhi waliyokuwa nayo ya kuongoza dunia na binadamu kwa ujumla imetanguliwa. Utenguzi wa uongozi kwa mayahudi ulitokana na mabaya yao waliyokuwa wakiyafanya na yale ambayo wanaendelea kuyafanya. Ujumbe huo unathibitisha wazi wazi kuwa uongozi huo umehamia kwa Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) achukue uongozi wa makao makuu ya 'Aqiydah ya Baba Ibrahimna pia kuwa makao hayo sasa ni Makkah na Msikiti wa Mbali (Al-Aqswaa) huko Al-Quds (Jerusalem). Hivyo mamlaka hayo yalihamishwa kwenda kwenye taifa ambalo ni la Wacha Mungu na lenye utii kwa Allaah pamoja na Mtume ambaye amependelewa kubeba Qur-aan ambayo inaongoza watu kuelekea kwenye ukweli. [Ibara imechukuliwa kutoka katika kitabu Ar-Rahiyqul-Makhtuum].

UCHAGUZI WA ASILI (FITWRAH)

Vyombo viwili vya dhahabu vililetwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), kimoja kikiwa kimejazwa maziwa na kingine kikiwa kimejazwa mvinyo (pombe). Jibril (عليه السلام) alimwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم) achague kinywaji kati ya hivyo vinywaji viwili. Mtume alichagua maziwa na akainua kile chombo na kuyanywa. Jibril alisema, "Umeongozwa katika fitwrah na umefikia daraja ya fitwrah. Kama ungelichagua mvinyo, watu wako wangelipotea." (Swahiyh Al-Bukhaariy Juzuu 6 Namba 232)

[Neno fitwrah lina maana ya silika asili ambayo imo kwa kila mtoto anapozaliwa, silika hiyo inamtambua Allaah Allaah; kama silika hiyo haikufisidiwa humpeleka mja katika Imani ya Tawhiyd ya Allaah.]

Imaam An-Nawawiy alisema kuwa kauli ya Jibril (عليه السلام) kwa Muhammad (صلى الله عليه وسلم), "Umechagua fitwrah" maana yake Mtume alikuwa amechagua dini ya Islam, yaani "Umechagua nembo ya Islaam na Istiqaamah (kuwa imara katika Njia Iliyonyooka). Maziwa yalikuwa ni alama tu kwa sababu ni rahisi kuyanywa wakati mvinyo ni "mama wa maasi na maovu" na chanzo cha matendo ya kikatili".

Kwa lugha nyepesi ni kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliletewa vitu viwili; kimoja kinawakilisha matendo mema na kingine kinawakilisha matendo maovu na viliwekwa mbele ye Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) na kwa silika akachagua kile kilicho kizuri. Kwa leo hii mtu akiacha fitwrah na kuanza kutafuta vitu vinginevyo anaonekana jinsi anavyohangaika baada ya kuacha njia ambayo amewekewa na Mola wake. Ni wajibu wa binadamu kushikamana na Njia ambaye ameamrishwa na Allaah kwa sababu, "Na atakayejiepusha na mawaidha Yangu, basi ya kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Qiyaamah Tutamfufua hali akiwa kipofu" (Twahaa 20:124)

"Na aliyekuwa hapa kipofu, basi atakuwa kipofu Akhera, na atakuwa aliyeipoteza zaidi Njia" (Al-Israa 17:72)

Mi'iraaj ni hali iliyomfikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) ya kupaa mbinguni kutoka Msikiti wa Al-Aqswaa na kwenda katika Mbingu na hata akawa amekutana na Allaah. Jibril (عليه السلام) alikuwa naye katika msafara huo wa kupaa. Ibn Kathiyr aliandika katika kitabu chake cha Al-Bidaayatu wan-Nihaayah: "Safari ya kupaa haikuwa kwa kutumia Al-Buraaq kwa sababu alikuwa amefungiwa katika mlango wa Baytul-Maqdis, akisubiri

Mtume akirejea kutoka mbinguni ili ampeleke Makkah."
Baada ya ziara ya Masjid Al Al-Aqswaa, Jibril (عليه السلام) na Mtume walianza safari ya kwenda mbinguni. Kila alipofika kwenye mbingu alibisha hodi na aliulizwa na walinzi wa mbingu hiyo, "Wewe nani?" na alipojibu kuwa ni "Jibril!" aliuliulizwa tena, "Nani umefuatana naye?" Alisema "Muhammad (صلى الله عليه وسلم)" Na aliulizwa tena, "Je ameitwa?" Na Jibril alijibu, Naam, Hakika ameitwa!" Na ndipo Malaika waliposema: "Marhaba, Anakaribishwa, Safari yake ni Njema kabisa." Milango ilifunguliwa na wakamwona Aadam (عليه السلام). Jibril alisema akimwambia Muhammad (صلى الله عليه وسلم), "Huyu ni baba yako Aadam (عليه السلام). Mpe heshima zake kwa salaam". Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimsalimu na Aadam aliitikia na
akasema, "Unakaribishwa Ewe Mwanangu Mtume Mtukufu" na akamwombea du'aa njema. Kisha walipanda mbingu ya pili na sawa kama hapo awali Jibril alibisha hodi na kuwaomba walinzi kufungua milango ya Mbingu na wakamuuliza maswali kama yale aliyoulizwa hapo mbingu ya kwanza. Hali ya namna hiyo iliendelea hadi kufika mbingu ya saba. Hatima milango ilifunguliwa na wakawa wamekaribishwa kwa kauli ya "Marhaba, Anakaribishwa, Safari yake ni Njema kabisa." Katika Mbingu ya pili Mtume alimwona 'Iysa bin Maryam (عليهم السلام) na Yahya ibn Zakariyah (عليهم السلام) mtu na binamu yake. Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) alisema, "Nilikutana na 'Iysa bin Maryam. Alikuwa na umbo la wastani na uso wake ni mwekundu kama vile katoka kuoga…" (Swahiyh Al-Bukhaariy Juzuu 4 Namba 647) Jibril alisema, "Hawa ni Yahya bin Zakariyah na 'Iysa (عليهم السلام) wasalimu", na Mtume aliwasalimu na wote wawili walijibu salamu zake na kusema "Unakaribishwa Ewe ndugu yetu Mtume Mtukufu" na kisha wakamwombea dua njema. Baada ya hapo walipanda Mbingu ya Tatu ambako walimkuta Yuusuf (عليه السلام) ambaye amejaliwa uzuri wa sura wa nusu ya dunia. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimsalimu naye akajibu salamu hiyo na akamkaribisha na akaondoka nao wakaenda Mbingu ya Nne pamoja. Milango ya Mbingu ya Nne ilifunguliwa na Idriys (عليه السلام) alikuwa hapo. Qur-aan inasema juu yake: "Na mtaje katika Kitabu Idriys. Hakika yeye alikuwa mkweli Nabii. Na Tulimuinua daraja ya juu". (Maryam 19: 56-57).
Idriys (عليه السلام) alimkaribisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) na wakasalimiana. Kisha Idriys aliondoka nao wakaenda Mbingu ya Tano ambako walimkuta Haaruun (عليه السلام). Mtume Haaruun (عليه السلام) aliwapokea na akajibu salamu zao na kumwombea dua njema Mtume (صلى الله عليه وسلم)
Kisha Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) alipelekwa Mbingu ya Sita ambako alimkuta Musa (عليهم السلام). Mtume anamsema, "Nilikuta na Musa (عليه السلام) nilipokwenda Mi'iraaj. Alikuwa ni mtu mrefu akiwa na nywele ndefu kama vile ni mtu wa kabila la Shanu (Swahiyh Al-Bukhaariy Juzuu 4 Namba 647). Musa (عليه السلام) alimkaribisha Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) na Jibril (عليه السلام), na wakasalimiana na walipoondoka kuendelea na safari yao, Musa (عليه السلام) alilia. Aliulizwa kwa nini analia basi Musa (عليه السلام) alijibu, "Nalia kwa sababu amepelekwa Mtume duniani baada yangu, kijana ambaye wafuasi wake wataingia peponi kwa makundi makundi zaidi ya watu wangu". Kisha waliendelea na safri yao kuelekea Mbingu ya Saba na huko wakamkuta Ibarahiym (عليه السلام) akiwa ameegemea Baytul-Ma'amuur (Nyumba ambayo inatembelewa mara kwa mara). Ndani ya nyumba hii kila siku wanaingia malaika 70,000 na wala hawarudi tena … na Mtume alisema, "Nilimwona Ibrahim (عليه السلام) ambaye mimi nafanana naye sana kuliko watoto wake wote" [Swahiyh Al-Bukhaariy Juzuu 4 Namba 647].
Ibrahimalimkaribisha Muhammad na wakasalimiana na Ibrahim(عليه السلام) akamwombea dua njema Mtume (صلى الله عليه وسلم) [Angalia maelezo ya Swahiyh Al-Bukhaariy Juzuu 5 Namba 227 na Swahiyh Muslim]
Ameeleza 'Abdullaah bin Mas'uud (رضي الله عنه) Mtume alisema, "Ndani ya usiku wa Mi'iraaj nilikutana na Ibraahim (عليه السلام) ambaye aliniambia, "Muhammad wapelekee Salaam zangu watu wako na waambie kuwa Pepo ni uwanda mpana ambao umeenea udongo safi, maji safi na miti yake hutoa sauti, "Subhaana Allaah, AlhamduliLaah La ilaha illa Allaah Allaahu Akbar." [At-Tirmidhiy namba 1445)

KITUO CHA MWISHO CHA SAFARI-SIDRATUL-MUNTAHAA

Amesema 'Abdullaah bin Mas'uud, "Wakati Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipochukuliwa safari yake kwenda Mbinguni alifikishwa mpaka Sidratul-Muntahaa ambapo kila kitu kinachopanda kutoka ardhini hukomea na na kile kinachoshuka kutoka juu hukomea hapo…" (Muslim 329).
RasuluLlaah akasema, "Kisha nilichukuliwa hadi Sidratul-Muntahaa mti ambao majani yake ni kama masikio ya tembo na matunda yake makubwa kama mitungi. Na mti huu ulipogubikwa na amri za Allaah, basi ulibadilika kuwa katika hali ambayo hakuna kiumbe ambaye anaweza kumsabihi Allaah kwa uzuri wake." (Muslim). Kisha katika riwaya nyingine: "Kisha nilipandishwa Mbinguni hadi kufikia Sidratul-Muntahaa. Matunda yake yalikuwa makubwa kama magudulia ya Hajr (sehemu ambayo ni karibu na Madiynah) na majani yake yalikuwa makubwa kama masikio ya tembo. Jibril (عليه السلام) akasema, "Huu ni mkunazi wa mbali kabisa" Kulikuwa na mito minne karibu yake miwili ikiwa haionekani na miwili ikiwa wazi inaonekana. Nikauliza, "Hii mito miwili ni mito gani? Ewe Jibril" Basi akajibu, "Ama kwa mito miwili isiyoonekana ni mito miwili ya Peponi na mito miwili inayoonekana ni mto wa Naili (Nile) na Furati (Euphrates)."
Hii hadiyth haina maana kuwa mito hiyo miwili inayoonekana kuwa asili yake ni Peponi, lakini ni kuonyesha tu mahali ambapo atakuwepo Mtume (صلى الله عليه وسلم) na watu daima watabakia wenye kushikamana na Uislamu na kurithishana kizazi kimoja baada ya kingine. (Ar-Rahiyqul-Makhtuum). RasuluLlaah (صلى الله عليه وسلم) pia alisema, "Jibril alinipandisha mbinguni hadi tukafika Sidratul-Muntahaa (mkunazi ambao una mpaka wa mwisho) ambao ulikuwa umepamba kwa rangi ambazo haziwezi kuelezeka. Kisha niliruhusiwa kuingia Pepopni ambamo nilikuta mahema (madogo madogo) au kuta ambazo zimejengwa kwa lulu na ardhi yake ilikuwa ni ya miski." [Al-Bukhaariy Juzuu 1 Namba 345].
Wakati nilikuwa natembea humo peponi (katika usiku wa Mi'iraaj) niliona mto na katika kingo zake kulikuwa na vijihema ambavyo vimejengwa kwa kutumia lulu zenye uwazi katikati. Niliuliza, 'Nini kile Ewe Jibril?' Akasema huo ndio mto wa Kawthar ambao Mola wako amekupa wewe. Basi harufu iliyotoka humo au kwenye matope ilikuwa ni miski. (Mmoja wa wapokeaji wa riwaya hii, Hudba hana hakina ilikuwa imetumika ibara gani.) [Swahiyh Al-Bukhaariy Juzuu 8 Namba 583]
"Katika usiku wa Mi'iraaj huko mbinguni pia nilimwona Maalik mlinzi wa Milango ya Motoni na Ad-Dajjaal miongoni mwa miujiza ambayo Allaah Alinionyesha huko."

[ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO]